

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
SHULE YA SEKONDARI SANTILYA**

SHULE YA SEKONDARI SANTILYA
S.L.P 1322,
MBEYA.
.....

Mawasiliano:

email: secondarysantilya@yahoo.com

simu: 0768013005 / 0658013006

Kumb.Na.MDC/SASS/S.1932

Kwa Mzazi/Mlezi wa.....

YAH: MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SANTILYA
KIDATO CHA KWANZA MWAKA

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na **Shule ya Sekondari Santilya** kidato cha kwanza kuanzia Januari 2021. Shule itafunguliwa rasmi tarehe saa

Kabla ya kuanza masomo yako unatakiwa kukamilisha mahitaji yako yaliyoandikwa katika fomu iliyoambatanisha.

Baada ya kukamilisha fomu tajwa hapo juu hakikisha unaita siku utakapokuwa unaripoti shuleni kwa mara ya kwanza uje na barua hii ya kuitwa kujiunga.

Aidha unatakiwa kuripoti shuleni bila kuchelewa tarehe ya mwisho kuripoti ni tarehe

Shule ya Sekondari Santilya iko Mbeya Vijijini kilomita zipatazo 40 kutoka makao makuu ya wilaya.

Hongera na **KARIBU SANA** Santilya sekondari.

.....
ELIUD L. SANGA
MKUU WA SHULE.
SHULE YA SEKONDARI SANTILYA

Nakala:-

- Afisa Elimu Mkoa,
S.L.P 754,
MBEYA.

- Afisa Elimu (W) Sekondari,
Halmashauri ya Wilaya Mbeya,
S.L.P 599,
MBEYA.

MAHITAJI YA LAZIMA

- (i) Kamusi ya kiingereza-kiswahili au kiingereza au zote mbili kwa pamoja
- (ii) Counter book tisa (9) za quire three kwa ajili ya nukuu (notes) ya masomo yako, mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical set), penseri, ruler na biki.

NB: Sare na mahitaji mengine vitakaguliwa siku ya kwanza kuripoti. Utarudishwa siku hiyo endapo hutatimiza masharti na mahitaji mengine yaliyoorodheshwa.

SARE YA SHULE

1. WASICHANA

- (i) Sketi mbili, moja rangi ya damu ya mzee na nyengine ya rangi ya kaki ya kuiva isiyopauka. zote ziwe tetron. Aidha sketi zote zisionyeshe mwili wa binti yako (transparent). Lazima sketi iwe ndefu, endapo itakua fupi atarudishwa mara moja kushona nyingine. Marinda ya sketi iwe ni nchi na nusu.
- (ii) Mashati (blauzi) mawili meupe aina ya tetron mikono mifupi mashati yawe marefu kwa ajili ya kuweza kuchomekea. Mashati yote yawe ya mviringo sehemu ya chini.
- (iii) Jozi mbili za viatu vyeusi (siyo raba) vya kamba. Viatu visiwe na visigino virefu au soli nene kupita kiasi.
- (iv) Soksi ndefu (stocking) nyeupe jozi mbili au zaidi.
- (v) Sweta rangi ya bluu na kushonwa vizuri isiwe ya wazi (not open) iwe na V-shape sehemu ya shingo.
- (vi) Raba jozi moja na nguo ya michezo.

2. WAVULANA

- (i) Suruali mbili, moja rangi ya damu ya mzee tetron na nyengine ya kaki ya kuiva tetron zisizopauka.
- (ii) Mashati mawili meupe aina ya tetron mikono mifupi na yawe marefu kuweza kuchomekea. Mashati yote yawe ya mviringo sehemu ya chini.
- (iii) Jozi mbiliza viatu vyeusi (siyo raba) vya kamba. Viatu visiwe na visigino virefu au soli nene kupita kiasi.
- (iv) Soksi ndefu (stocking) nyeusi jozi mbili au zaidi.
- (v) Sweta rangi ya bluu na kushonwa vizuri isiwe ya wazi (not open) iwe na v-shape sehemu ya shingo.
- (vi) Raba jozi moja na nguo ya michezo.
- (vii) Mkanda mweusi usio na maandishi au picha.

NB: Napenda kuwatahadharisha kuwa mzazi/mlezi yeyote ambaye atamnunulia mtoto wake sare isiyotakiwa, atalazimika kununua nyingine kadri ya maelekezo.

NAKUTAKIA UTEKELEZAJI MWEMA NA KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SANTILYA.